

Taasisi ya Thirdmill

Beji ya Uwakili

“Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. Hapo tena inavyohitajiwa katika mawakili, ndivyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.”

1Wakorintho 4:1-2.

Uwakili ni moja ya mada muhimu zaidi kwenye Biblia, na maelfu ya vifungu vinahusiana na Uwakili. Mafundisho ya uwakili kibiblia yanafafanua uhusiano wa mwanadamu kwa Mungu. Inamtaja Mungu kama mmiliki na mwanadamu kama mtawala. Mungu anamfanya mwanadamu kuwa mfanyakazi mwenzake au msimamizi katika kusimamia vipengele vyote vya maisha yetu. Mungu ametupa wajibu wa kusimamia uumbaji wake tangu mwanadamu alipoingia Duniani kwa mara ya kwanza. Kwenye beji hii, tutachunguza inamaanisha nini kuwa msimamizi wa ki-Mungu. Tunao wajibu wa kuwa wasimamizi wazuri wa mambo mengi – muda wetu, vipaji vyetu, hazina zetu, miili yetu kama hekalu la Mungu, makundi ya mifugo, fedha zetu. Kila mmoja wetu ana jukumu katika usimamizi wa Ufalme wote wa Mungu.

Vipengele vya Beji:

Uwakili wa ki-Biblia – Biblia inatufundisha nini kuhusu uwakili?

Kuchunguza Uwakili wetu– Ni kwa namna gani Mungu anaitu tuwe wasimamizi waaminifu zaidi?

Tamaduni na Uwakili– Ni wapi tamaduni zinakinzana na uwakili wa kibiblia na tunawezaje kuziba pengo hilo.

Mada za kujadili

1. Kutokana na kujifunza kwako Maandiko kuhusu uwakili, Jadili baadhi ya mambo tofauti tofauti ambayo Mungu ametuitia kuyasimamia. Taja maeneo yote ambayo Mungu anampa mja wake kuyatunza chini ya Ufalme wake.
2. Kutokana na Maandiko uliojifunza juu ya uwakili, jadili jambo jipya ulilojifunza ambalo Mungu anatataraajia sisi kulisimamia? Unajisikiaje kuhusu wajibu huu?
3. Soma Matayo 25:14-30. Fikiria eneo ambalo ulilisimamia vizuri na ukapewa jukumu zaidi. Fikiria eneo ambalo hofu ili kufanya usisimamie vizuri. Jadili mfano wa simulizi hiyo na linganisha uzoefu wa maisha yako na mmoja wa watu hao watatu waliopewa talanta katika mfano wa simulizi hiyo.

4. Tito 1:7 Inawataka mawakili wawe watu wasiolaumiwa. Jadili namna tabia binafsi inavyohusiana na uwakili.
5. Pamoja na kikundi chako jadili wapi Mungu anawataka ninyi muwe wasimamizi waaminifu zaidi. Ni Kwa namna gani wana kikundi wenzako wanakusaidia katika safari ya kuwa msimamizi bora?
6. Malaki 3:10 inasema kuwa Mungu ni mwaminifu tunapokuwa waaminifu na zaka zetu. Jadili uzoefu wako kuhusu zaka kama inavyohusiana na mstari huu.
7. Luka 14:28 inatufundisha kwamba tuwe na uhakika wa kuwa na rasilimali za kumaliza jambo kabla hatujalianza. Jadili ni wapi umeona kanuni hii ikifuatwa na matokeo yake ya ushindi, na wapi palitoa matokeo ya kushindwa pale kanuni hii haikufuatwa.
8. 1Wakoritho 6:20 Inasema kuhusu uwakili wa miili yetu. Jadili baadhi ya njia ambazo Mungu anatutaka tuwe wasimamizi wa miili yetu katika mambo tunayopaswa kuyafanya na mambo tusiyoapaswa kuyafanya.
9. 1 Mambo ya Nyakati 29:11-12 inasema kuwa kila kitu ni cha Mungu. Jadili eneo katika maisha yako ambapo unategemea nguvu zako kuliko nguvu za Mungu.
10. Mambo ya Walawi 23:3 Inahusu Sabato. Jadili namna ambavyo mafundisho ya kibiblia kuhusu Sabato yanahusiana na uwakili.
11. Matayo 6:24 inatufundisha jinsi ambavyo hatuwezi kutumikia mabwana wawili. Katika kusoma tamaduni na uwakili, ni wapi unaona waumini wamegawanywa kati ya mabwana wawili? Ni kwa namna gani hii inaweza kushughulikiwa ili waumini wamtumikie Mungu pekee?

Mambo ya Kufanya:

1. Tafuta vifungu kumi kwenye Biblia vinavyohusu uwakili. Vifungu hivi ni lazima vionyeshe maeneo tofauti ya uwakili, kama vile uwakili wa miili yetu, uwakili wa pesa, uwakili wa makundi ya mifugo yetu, uwakili wa familia zetu, na uwakili wa Ufalme wa Mungu. Orodhesha vifungu ulivyoona na kutafakari katika vifungu hivi.
2. Omba utambuzi juu ya eneo la maisha ambalo Mungu anakutaka uwe msimamizi bora. Endeleza mpango wa uboreshaji katika eneo hili. Hakiki mpango huu na mkufunzi wako kabla ya kuutekeleza na tena baada ya mwezi mmoja wa utekelezaji wa mpango huu.
3. Kama ulivyosoma uwakili wa Kibiblia, ainisha mahali ambapo tamaduni yako inakinzana na sauti ya uwakili wa Kibiblia. Ainisha mafundisho kutoka kwenye Biblia ambayo yanaweza kutumika kuwafundisha wengine kuwa imani za kitamaduni hazimuheshimu Mungu na zinapaswa kubadilishwa. Shirikisha mpango wako wa

ufundishaji na mkufunzi wako au wanakikundi wenzako na kisha ufundishe waumini wenzako.

Vigezo vya Beji:

Utatunukiwa Beji hii na taasisi ya Thirdmill kama sehemu ya Cheti cha Misingi baada ya kufuzu vigezo vyote vya Beji vilivyo kwenye ***mambo ya kufanya*** kwa uaminifu, na ***uthabiti***, kwa kufuata ***vipengele vya Beji***, na muktadha wa ***mada zilizozungumziwa*** katika kipindi chote cha kozi.